JE! UNA UHAKIKA
KWAMBA UNAO

UZIMA WA MILELE

NA KWAMBA UTAENDA
MBINGUNI UTAKAPOKUFA?

Mungu Anataka Uwe na Hakika.

Biblia inasema kwamba, “Nimewaandikia nyinyi mambo haya, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele nyinyi mnaoliamini jina la Mwana wa Mungu” (1 Yohana 5:13).



Fikiria Swali Hili Pia:

Ikiwa sasa hivi umesimama mbele ya Mungu na akuulize, Je! kwa nini unataka nikuruhusu uingie mbinguni?” **Unafikiri utamjibu vipi?**

Pengine hutajua la kusema lakini . . .

Unaweza kujua kwa sababu Mungu anatupenda na ana kusudi na maisha yetu.

Biblia inatwambia hivi,
“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wapekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16).



KUSUDI LA MUNGU NI KWAMBA TUWE NA UZIMA WA MILELE.

- **Tunapokea uzima wa milele kama zawadi.**

"Bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu" (Warumi 6:23).

- **Sasa hivi tunaweza kuishi maisha ya maana na yenye ukamilifu.**

"Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele" (Yohana 10:10).

- **Tutaishi na Yesu milele mbinguni.**

"Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu, ili nilipo mimi nanyi mwepo" (Yohana 14:3).

Uzima wa milele huyafanya maisha yetu kuwa ya maana sasa hivi.

Hali . . .

Utu wetu wa dhambi hutuzuia kutimiza kusudi la Mungu maishani mwetu. Hivyo basi . . .

TUNAHITAJI KUELEWA SHIDA YETU.

- **Sote tuna dhambi kwa uamuzi na asili yetu.**

"Kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23).



- **Hatuwezi kujiokoa sisi wenyewe.**

"Wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu" (Waefeso 2:9).

- **Sisi tunastahili mauti na jehanam.**

"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti" (Warumi 6:23).

Ni Kweli Kwamba:

Mungu ni mtakatifu na mwenye haki na ni lazima aadhibu dhambi, vile vile anatupenda na ametoa msamaha wa dhambi zetu. Yesu akawaambia, "Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima, mtu haji kwa baba ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6).

Habari Njema ni kwamba Mungu ametoa msamaha wa dhambi zetu.



TOLEO LA MUNGU KWETU NI YESU KRISTO.

- **Yesu ni Mungu na alizaliwa kama mwanadamu.**

"Hapo mwanzo kulikuweko Neno, naye Neno alikuweko kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu" (Yohana 1:1,14).



- **Yesu alikufa msalabani kwa ajili yetu.**

"Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu" (1 Petro 3:18).

- **Yesu alifufuliwa katika wafu.**

"(Yesu) ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tupate kuhesabiwa haki" (Warumi 4:25).



Hiyo ni habari njema, . . . lakini njia pekee ambayo Yesu anaweza kubadilisha maisha yetu ni kwa kumpokea.

Biblia inasema kwamba, "Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu ndio wale waliaminio jina lake" (Yohana 1:12).

Uamuzi ni wetu. Kwa hiyo . . .

ITIKO LETU NI KUMPOKEA YESU.

- **Ni lazima tutubu dhambi zetu.**

“Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe” (Matendo 3:19).

Kutubu siyo kusikitikia dhambi zetu tu. “Watubu na kumwelekea Mungu wakiyatenda matendo yanayopatana na kutubu kwao” (Matendo 26:20).

Kutubu ni kuacha dhambi zetu kabisa na kumgeukia Mungu kupitia kwa Yesu. Ni kugeuka hivi (angalia mchoro).



Tunapogeuka . . .



- **Ni lazima tumwamini Yesu Kristo.**

"Kwa maana mmeokolewa kwa neema kwa njia ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu" (Waefeso 2:8).

Imani siyo kuamini mambo kuhusu Yesu tu. "Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja, watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka" (Yakobo 2:19).

Imani ni kumwamini Yesu. Ni kama kusafiri na ndege. Huwezi kusafiri mpaka utakapoamini na kuingia.

MASWALI MATATU MUHIMU:

- **Je! uliyoyasoma yana maana kwako?**
- **Je! kuna sababu yo yote ambayo itakufanya usiipokee karama ya Mungu ya uzima wa milele?**
- **Je! uko tayari kuacha dhambi zako na kumwamini Yesu sasa hivi?**

Biblia inasema kwamba, “Kwa kuwa kila atakayeliita jina la Bwana ataokoka” (Warumi 10:13).

Unapaswa kumwomba Bwana akuokoe.

Tafadhali soma sala hii uone kama ndivyo unataka kumwambia Mungu.

Bwana wangu, nimeamini kwamba wewe ni Mwana wa Mungu, na kwamba ulikufa msalabani na kufufuliwa katika wafu. Ninajua kwamba nimefanya dhambi na ninahitaji msamaha. Nimeacha dhambi zangu zote na kukupokea uwe Bwana na mwokozi wangu. Asante Bwana kwa kuniokoa.

Mwite Bwana na kutubu, kwa imani, na kujitoa, kwa kutumia maneno haya na Yesu atakuwa Bwana na Mwokozi wako.

Karibu katika jamaa ya Mungu. Umefanya uamuzi muhimu wa maisha yako.

KUMWAMINI YESU KABISA, MAANA YAKE . . .

• Ni lazima kumfanya Yesu kuwa Bwana.

“Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana . . . kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu” (Warumi 10:9-10).

Yesu kuwa Bwana siyo kusema tu kwamba tunampa Yesu maisha yetu. “Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba aliye mbinguni” (Mathayo 7:21).

Kumfanya Yesu kuwa Bwana ni kumruhusu atawale maisha yetu.

Kumruhusu Yesu atawale maisha yetu ni kama kutembea njiani na mtu mwingine. Ikiwa unajua njia wewe ndiye kiongozi. Lakini unapofika mahali fulani na kutambua kwamba hujui njia, na mwenzako anaifahamu, unamwambia, “Wewe ongoza sasa.” Huyo mwenzako ndiye anayetawala. Wewe utafuata njia anayoichagua.

Thibitisho la Yesu kutawala maisha yako ni kwamba utataka *kujifananisha* naye. Njia ya Agano Jipya ni kumkiri Yesu mbele ya watu (Mathayo 10:32-33) na kumfuata katika ubatizo na kuwa mshiriki wa kanisa (Matendo 2:41).

UNAWEZA KUWA NA HAKIKA KWAMBA UMEOKOKA NA UNAO UZIMA WA MILELE KWA SABABU . . .

Mungu hutimiza ahadi zake.

- Umetubu dhambi zako (Matendo 3:19).
- Umemwamini Yesu (Waefeso 2:8-9).
- Umemkubali Yesu kuwa Bwana (Warumi 10:9-10).

Mungu amesikia ombi lako.

“Kwa kuwa, kila atakayeliita jina la Bwana ataokoka” (Warumi 10:13).

Mungu ameandika kujitoa kwako.

“Furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni” (Luka 10:20).

Unahitaji kukua kama Mkristo.

Biblia inawaita Wakristo wapya “watoto wachanga katika Kristo” (1 Wakorintho 3:1).

Watoto hawatakua bila ya kupewa vitu muhimu.

Kanisa kwa Mkristo mpya ni kama nyumba na jamaa kwa mtoto mchanga.



Unajiunga na jamaa yako mpya kwa kumkiri Yesu mbele ya watu na kushiriki katika ubatizo wa waamini. “Nao waliolipokea Neno lake wakabatizwa, na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu” (Matendo 2:41).

Hudhuria kanisa na umwambie mchungaji wako kwamba unataka kubatizwa na uwe mshiriki wa kanisa.

Mkristo mpya anahitaji **kuomba** jinsi mtoto mchanga anavyohitaji kupumua. Nilazima apumue daima.

Biblia inasema kwamba, “Ombeni bila kukoma” (1 Wathesalonike 5:17).

Jifunze kuomba kwa kutaja mahitaji yako. “Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote” (1 Yohana 1:9).

Mkristo mpya anahitaji **Neno la Mungu** jinsi mtoto mchanga anavyohitaji chakula bora. Chakula bora kinahitajika kila siku ili mtoto akue vizuri. “Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshwa ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu” (1 Petro 2:2).

Mkristo mpya **hujifunza kushuhudia** jinsi mtoto mchanga anavyojifunza kuzungumza.

Kristo ametuamuru tueneze habari njema kwa wengine. “Nanyi mtakuwa mashahidi wangu” (Matendo 1:8).

Andika jina la mtu ambaye atafurahi kujua uamuzi wako wa kumfuata Kristo_____, na jina la mtu ambaye anahitaji kumpokea Kristo_____.

Je! utawaambia kuhusu maisha yako mapya?

Nimempokea Kristo _____

(Tarehe)

_____

(Jina)

CHETI CHA KUZALIWA CHA UZIMA WA MILELE

“Furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni ” (Luka 10:20).

Mimi, _____ nilimpokea

Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi _____ (saa)

mnamo _____ (tarehe).

Mtu aliyenihubiria ujumbe wa Kristo:

_____.

“Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele ya Baba yangu aliye mbinguni.” (Mathayo 10:32).

Kata hapa

FOMU YA MAAMUZI

Tarehe ya Leo: _____

Jina _____

Anwani _____

Mji _____ Nchi _____ ZIP _____

Simu (_____)_____- _____ Jinsia _____

Tarehe ya Kuzaliwa _____

Umri: ___1-11 Mtoto ___ Kijana 12-17
___18-30 Mtu mzima ___31-50 Mtu mzima ___51+ Mtu mzima

Hadhi ya Ndoa: ___Pweke ___Nimeoa/lewa ___Mjane/mjane mwanaume

Jina la mkeo/mumeo: _____

Kanisa Linalofadhili _____

___ Nilimpokea Kristo ___ Nilijitoa upya
___ Nitajiunga katika mafundisho ya Biblia
___ Niko tayari kutangaza imani yangu hadharani
Matamanio ya Kanisa? ___N ___L
Kiwango 1, 2, 3. (1 ndiyo bora zaidi.)

Wakati mzuri zaidi wa kukufikia nyumbani kwako:_____

Historia ya Kidini _____

Kabila lako _____

(Tafadhali mpa karatasi hii mchungaji au kiongozi, au itume kwa anwani iliyopo upande wa pili wa fomu hii.)

Pendekezo: weka kibandiko cha anwani ya kanisa lako kwenye anwani uliyopewa

Iweke ndani ya bahasha
na uitume fomu hiyo kwa:

People Group/Interfaith Evangelism Team
North American Mission Board
4200 North Point Pkwy.
Alpharetta, GA 30022-4176

VIDOKEZO KWA MWAMINI MPYA

Kuna adui. Yesu alisema, “Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu” (Yohana 10:10). Shetani hakuweza kukuzuia kumpokea Kristo, kwa hiyo sasa atajaribu kukuzuia kuwa mfuasi wa Kristo mwenye furaha, na mwenye nguvu. Tarajia upinzani.

Lakini una rafiki. “Lakini yuko rafiki aambatanaye na mtu kuliko ndugu” (Mithali 18:24). Yesu alisema, “Tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari” (Mathayo 28:20).

Ukiwa na Kristo wewe ni mshindi! “Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia” (1 Yohana 4:4).

For more information about your new life in Christ, contact us at
1 888 JESUS 2000 or *www.thegoodnews.org*

TUNA KUJALI.

Jina langu ni: _____ Simu: _____

Jina la kanisa, anwani, na simu:

North American Mission Board
4200 North Point Pkwy.
Alpharetta, GA 30022-4176

A Southern Baptist Convention agency supported by the Cooperative Program and the Annie Armstrong Easter Offering®
For general information, call (770) 410-6000 or visit *www.namb.net*. To order materials, call Customer Service Center, 1 866 407-NAMB (6262), fax, (770) 442-9742, or visit *www.nambstore.com*.

ISBN# 22.084008787X

0803071/10M/06-09 (Swahili Edition)